# MTIHANI WA KANDA YA BUKAKA

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**
**KISWAHILI 102/3**
**KIDATO CHA NNE**
**MWISHO WA MUHULA WA KWANZA**

1. Shairi

**a.** Binadamu hatosheki/ binadamu ana tamaa/tamaa ni hatari.(1x1)

**b.**

1. Mtu aliye na tamaa huwa hatari kama nyoka
2. Unafiki wa mtu asiyeaminika
3. Masengenyo
4. Balaa ya kumkirimu mchawi ni kutupiwa kinyesi (4x1)

**c.i.** Ukawafi – Kila mshororo una vipande vitatu – ukwapi, utao, mwandamizi

**ii.** Ukaraguni –vina vya kila kipande vinatofautiana katika shairi nzima.

**iii.** Tarbia – Kila ubeti una mishororo minne. (3x1)

**d. ubeti wa nne kwa lugha nathari**

Ni taabu kuishi na mtu aliye taraghani kwani kazi yake ni kujidai.Atakusema faraghani asivyosema ukiwa naye kuwapendeza maadui zako.Ni mtu akuchimbaye. Hana faida nyumbani bora usimtegemee. Mtu aliye na tamaa ya kutaka kisicho chake ni hatari kama nyoka.

**e.**

1. Tashbihi/tashbiha – ni hatari kama nyoka
2. Tashihisi/uhaishaji/uhuishi – bahati inahadaa bahati kupewa uwezo wa kudanganya
3. Litifati – Subutu' kumwacha mtu ajisemee
4. Jazanda /sitiari Kinyesi nimetupiwa (2x1)

**f.**

**1.** Inkisari – ukweliye badala ya ukweli wake, kiso badala ya kisicho n.k

**2.** Miundo ngeu ya kisintaksia/ kuboronga sarufi/kufinyanga sarufi – ninacho changu kilio badala ya ninacho kilio changu.(2x1)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**g.**

1. Urudiaji wa neno – kweli
2. Urudiaji wa sauti – a-balaa, hadaa, jaa, tamaa
3. Urudiaji wa mstari- mtu kuwa na tamaa. Akitaka kiso chake. Ni hatari kama nyoka
4. Urudiaji wa silabi – Ki, ki, ki (2x1)

**h.**

**1.** Mistari/mishororo minne katika ubeti
**2.** Vipande vitatu katika kila mshororo
**3.** Vina vyake ni: a, wi, yo
**4.** Mizani 8,8,8 = 24 katika kila mshororo
**5.** Mshororo wa mwisho unarudiwarudiwa/kibwagizo (lazima atolee mfano mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake,ni hatari kama nyoka. (3x1)

2.

Msemaji ni Bela

Msemewa ni Neema

Walikuwa nyumbani kwa Neema na Bunju.

Ni baada ya Neema kumwambia eti wazazi wake hawawezi kulala kwa mpwa wao.

Ndipo Bela akajibu- hayo ni ya kale.

b) Mdokezo-ya kale…

Uradidi- ya kale

Mdokezo wa methali-…ya kale hayaachi kunuka

Taswira (mnuso)- hayanuki

c) Msemaji ni Bela

**sifa za Bela**

1. Mwenye busara/ mshauri mwema-Anampa Neema mashauri kuhusu maisha.

2. Mtu wa kutegemewa- Ana uhusiano mwema na mwajiri wake na anaelewa kazi yake vizuri. Anamkumbusha Neema kuhusu kazi za shule za Lemi kwani, anaelewa jukumu lake la kuwalea watoto wa Neema.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

3. Mlezi mwema. Bela analea watoto wa Neema vizuri na kwa bidii.

4. Mwenye bidii: Bela anafanya kazi ya kuwalea watoto wa Neema kwa bidii

d. Jadili maudhui ya utamaduni kama yanavyojitokeza katika Tamthilia nzima. (al.9)

-Jamii inayorejelewa kwenye tamthilia inashikilia mila na tamaduni. Mtoto wa kiume anatukuzwa kama mrithi. Mfano katika ndoa ya Sara na Yona

-Mtoto wa kwanza ana jukumu la kuwasaidia wazazi wake. Kwamba fimbo ya mzee hurithi mtoto wa kwanza.

-Mama mkwe hawezi kulala kwa mkazamwanawe. Sara hawezi kulala kwa Bunju kutokana na utamaduni.

-Enzi za kitambo wasichana hawakupewa elimu. Mfano Sara

-Jamii hii inashikilia utamaduni wa wazee kukutana baada ya mavuno ya kwanza na kutoa Baraka.

-Luka anasema mavuno ya kwanza huonjwa na wazee na kutoa Baraka.

-Beni, Luka pamoja na wazee wenzake wanalalamika kuwa kizazi cha sasa kimetupa mila.

-Watoto wa sasa hawajui lugha yao ya mama

-Mume hafai kufanya kazi za nyumbani hasa za jikoni. Mfano Yona

-sara anamwambia Asna kuwa anataka atafute atakayemletea leso

**3.** "...Hebu fikiri umepata ajali mbaya. Inakuacha mahututi. Anapita mtu katika gari lake. Kwa Imani anaguswa. Anakufanyia mpango wa Flying Doctors, ndege inafika inakupeleka hospitali. Mwenyewe huyo anakulipia kila kitu! Mtu huyo atakosaje kuwa zawadi kwako?"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b) Tambua umuhimu wa mbinu zozote mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (al.4)

c) Eleza umuhimu wa anayerejelewa katika dondoo hili. (al.4)

d) Kwa kutoa hoja zozote nane kutoka kwa tamthilia nzima. Eleza ukweli wa kauli, 'mtu huyo atakosaje kuwa zawadi kwako?'(al.8)

a) maneno ya Neema anajisemea.

b) yuko nyumbani kwake

c) ni baada ya Neema kumuomba Bunju amsaide kulipa gharama ya hospitali ya mamake Sara, ila Bunju anamwambia hataweza kwa kuwa ana madeni chungu nzima.

d) Nidaa-Hebu fikiri!

Kuonyesha hisia

Swali balagha-atakosaje kuwazawadi kwako?

Kusisitiza ujumbe

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

e) mrejelewa ni Bunju

-ni kielezo cha wanaume wanaowajibika katika jamii
--anaonyesha matatizo yanayokumba ndoa
-ni mfano wa wanaume wanaofanya mambo kisiri katika ndoa
- ametumika kupiga tamaduni hasi
-ametumiwa kuchimuza maudhui ya mgogoro wakati wanajadiliana kuhusu alama za Lemi.
-anaendeleza ploti

f) -kumununulia gari
-kuwajengea wazazi wa Neema nyumba
-kugharamia majukumu yote ya nyumbani
-kusaidia Neema kulipa gharama yote ya hospitali ya Sara
-kumfanyia Neema mpango wa flying doctors
-kumlipia Neema gharama za matibabu
-kuwasomesha wanuna wa Neema
-kumpa Neema uhuru wa kutumia pesa zake atakavyo.
-anamsaidia Lemi kufanya kazi ya ziada

4 a) mzimu wa Kipwerere

a) Eleza aina ya taswira katika kifungu hiki.

**Taswira mwendo**- Hapo nikasogea karibu zaidi na …

- ✓ **Taswira oni/muono**-nilichokiona humo, sikuamini macho yangu!/nikaangalia huku na huko
- ✓ **Taswira mnuso**-asumini na maua ya mlangilangi./ chang'aa na tembo ya mnazi
- ✓ **Taswira sikivu**- nikauimba ule wimbo wote
- ✓ **Taswira hisi**-nikajitoma kichakani mle bila hofu wala kimeme(4x1)

b) Ukirejelea hadithi ya ***" Mzimu wa Kipwerere***," Fafanua jinsi imani katika mambo ya kichawi yamejikita katika jamii. (al 6)

Ni imani potovu kuhusiana na masuala ya ramli, uchawi, mizimu na masuala ya aina hiyo.

i. Inaaminika kwamba Kipwerere alimpata **shetani aliyefichua damu**.Hii ndio maana Kichaka hiki cha kutisha kinachohusiana na matendo yakishetani kikapewa jina Mzimu wa Kipwerere kwani jamaa huyu alizikwa hapa

ii. Pia,haikuruhusiwa mtu **kupita karibu na kichaka hiki cha kutisha majira ya saa sita mchana**.Iwapo kuna mtu atathubutu kupita hapo wakati huo basi atakufa na kutolewa kafara.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

iii. Kwa kuongezea, **hakuna mtu aliyeruhusiwa kupita pale majira ya usiku**.Inasemekana kuwa wakati huo ndipo mashetani wanaoishi kwenye msitu huo wanafanya shughuli zao. Kwa hivyo, iwapo utavunja miiko hii basi utakufa.

iv. pia, **hakuna mtu aliyeruhusiwa kuingia kwenye msitu** huo kama si mmoja kati ya Wazee wa mji au wale wanaojiita wahenga waliotukuka.Ukithubutu kuingia humo ndani basi utakutana na mashetani watakao kufanya mali yao.

v. Inaaminika kuwa unapopita hapo na usikie watu wakiongea;mume na mke,**basi ujue kwamba shetani pia ana mke** na wako katika harakati zao za kupanga mipango yao.

vi. Pia **kuongea kwa hawa mashetani kwa sauti ya chini** kunaishiria kuwa watoto wao wamelala.Kwa hivyo wanatumia fursa hiyo kushauriana na kupanga mikakati yao ya kuendeleza maisha.

vii. Unapopita karibu na mzimu na usikie harufu kali ya sigara, **basi inaaminika kuwa shetani pia wanavuta sigara.** Kwa hivyo wakati huo wanavuta sigara.Katika kijiji hiki Salihina ndiye aliyeruhusiwa **kufanya kimila kama vile matambiko** iwapo kuna mwanakijiji yeyote amekumbwa na jambo .

viii. Pia iwapo kuna **watoto wanaotaka kupashwa tohara ni lazima waletwe** pale mzimuni ili kuombewa na kupewa baraka na Salihina. Mizimu ikikubali shughuli hiyo ifanyike basi, itafanyika bila madhara yoyote.

ix. Inaaminika kuwa **kukiwa na harusi au sherehe yoyote** kijijini ni lazima Salihina azungumze na mizimu ili hiyo sherehe ifane.

x. Mtu anapotaka **kuingia mzimuni ni lazima awe na ufunguo**. Ufunguo ambao ni wimbo.Ni wale watu wanaojua kuuimba tu ndio wanaoweza kuingia mzimuni. Ilimlazimu msimulizi kujifunza wimbo huu ndipo aweze kuingia kwenye msitu huu.

xi. **Ulaghai kwa sababu ya ushirikina-** Kuna wimbo unaoaminiwa kuwa ufunguo wa kuingia mzimuni. Anausikia kutoka kwa Salihina na kuuimba kisha kuingia. La kushangaza ni kuwa hamwoni shetani yeyote anavyotarajia.Anagundua kuwa Salihina ndiye anaendesha shughuli zote wanazoshuhudia msituni humo.

xii. **Mihadarati kuuzwa huku walanguzi wakitumia woga wa mzimu**-Salihina na Bishoo wanatumia itikadi na imani potovu kuchuuza mihadarati. Bishoo anamweleza mpango wake wa kusafirisha dawa hizo kwa kubeba ndoo wanazodai kuwa wanaenda kuchotea shetani wa mzimu maji. Hata polisi wenyewe wanawaruhusu! Ndoo hizo hatimaye zinajazwa ‘mzigo’; mihadarati.

**4c**. )Katika hadithi ya **Msiba wa kujitakia na D.W.Lutomia** athari za uteuzi

mbaya wa viongozi zinaoenkana wazi. Zitambue. (alama 10)

- ✓ **Ukosefu wa ajira-Machoka anatafuta kibarua mchana kutwa na anaambulia patupu**
- ✓ **Njaa/ukosefu wa chakula-matumbo ya Machoka yanateta kwa kushindwa kuhimili njaa**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

- ✓ **Utabaka-maisha ya wapiga kura na wapigiwa kura ni tofauti**
- ✓ **Mfumuko wa bei za bidhaa-bei ya bidhaa iliongezeka kinyume na matarajio ya wanamatopeni baada ya uchaguzi**
- ✓ **Kutozwa ushuru wa kiwango cha juu-serikali iliendelea kuwatoza wanamatopeni ushuru wa juu wa mishahara yao duni kuwasukumia kuwa maskini zaidi**
- ✓ **Mshahara duni-mwandishi anasema kwamba mishahara yao duni iliwasakama kwenye udhalimu**
- ✓ **Wizi wa kura-kwamba Matopeni kuhesabu kura ndio muhimu kushinda kupiga kura**
- ✓ **Kulimbikiziwa viongozi-wanamatopeni hulimbikiziwa viongozi wasiowataka**
- ✓ **Ubadhirifu wa mali ya umma-Sugu Junior anatumia mamlioni ya pesa ya umma kugharamia nauli ya ndege kwa viongozi wa majimbo.**
- ✓ **Ukabila -Zuhura anasema kuwa watamchagua mtu wao**

**Zozote 10*1=10**

**5.**

a. Tambua na ueleze toni ya dondoo hili. (al 2)

**Toni ya furaha- Ombati anamwita mwanawe Mike kushangilia matokeo ya mtihani akidhani ni yake.**

b. Changanua mtindo katika dondoo hili. (al 2)

**Nidaa- mike!**

**Mdokezo-mwanangu…**

**Uradidi -Mike! Mike!**

c. Eleza sifa nne za msemaji wa dondoo hili. (al 4)

1. **Ni mwenye tamaa. Ananuia kujinufaisha kutoka kwa dadake kupitia kwa mahari yake. Anapoyakosa, anaamua kutumia bintiye, Sabina, kwa kumwoza baada ya darasa la nane ili kupata mifugo.**
2. **Ni mtamaduni. Anaendeleza mifumo ya kijamii kama vile ubidhaaishaji wa wanawake. Anataka kupata mahari kupitia kwa Nyaboke na anapoyakosa,**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**anaamua kumwoza bintiye, Sabina, katika umri mchanga na kumwandalia sherehe. Anasemekana kumlaani Nyaboke kwa kumkosesha mahari.**

**3. Ni kigeugeu. Maripota wanapofika kumhoji Sabina, anaungana naye huku akijisifia jinsi alivyomlea na alivyo mwerevu, licha ya kuwa awali anamtelekeza. Anawafukuza waliokuja kumposa Sabina na mifugo wao.**

**4. Ni mwongo . Anamhadaa mwalimu mkuu kuwa Sabina anapata muda wa kutosha kujiandaa kwa ajili ya mtihani. Anadanganya kuwa Sabina anapenda kazi za shambani hali analazimishwa.**

**5. Msaliti- anaisaliti jamaa yake kwa kumwacha Yunuke kumtesa mwana wa dadake Nyaboke.**

**6. Mbaguzi- anabagua kati ya wana wake na mtoto wa dadake Sabina. Sabina anatumikizwa huku wanawe wakikaa starehe.**

**7. Ni katili-anamlazimisha Sabina Kwenda shambani ilhali wanawe wanastarehe.**

**8. Ni mnafiki-anamtelekeza Sabina badala ya kumtunza kama mjomba wake.**

Za kwanza 4x1=4

d. Eleza mbinu mbili ulizozitumia kutambua sifa za msemaji wa dondoo hili. (al 4)

**-Usawiri wa mwandishi**

**-Maneno ya wahusika wengine**

**-Maneno yake mwenyewe**

**-Matendo yake kwa wahusika wengine**

e. Tambua na ufafanue madhila yanayomsakama mhusika mkuu katika hadithi hii ya “Sabina”. (al 8)

**-Kufiwa na mamake Nyaboke na kuachwa mikononi mwa babu na nyanya yake.**

**-Babu na nyanyake kufariki akiwa darasa la tano. Hili linamfanya achukuliwe na mjombake Ombati na Yunuke.**

**-Alitumikizwa sana nyumbani kwa mjombake ambako alifanya kazi za kila aina.**

**-Anapokea kichapo kutoka kwa Yunuke baada ya kuchelewa kutoka shuleni.**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**-Anatusiwa sana na Yunuke. Anaitwa baradhuli, kiokote,mjalaana n.k.**

**-Kusingiziwa. Sabina anasingiziwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamume Fulani.**

**-Kubaguliwa. Binamu zake wanasomea shule za bweni huku yeye akisomea shule ya kutwa.**

**-Kunyimwa nafasi ya kudurusu. Yunuke anazima kibatiri hivyo kumnyima Sabina nafasi ya kumalizia kusoma alichokuwa amebakisha.**

**-Kuozwa.mjombake Ombati anapanga kumuoza kwa kijana mwendesha pikipiki hivyo kuzima ndoto yake ya kuendelea na masomo.**

**-Kupuuzwa- yunuke na Ombati waliziona juhudi zake masomoni kama za bure.**

**-Kukosa malezi ya wazazi wote. Babake anamringa mimba mamake Nyaboke na kumtoroka**.

**6.** NGUU ZA JADI

a) **Weka maneno haya kwenye muktadha wake. (alama 4)**

Mbungulu anaambia Waketwa wenzake wakiwa nje ya kanisa. Anashuku kuwa huenda Mbwashu akatumia fursa hii kuwauzia bidhaa za kiwanda chake.

b) **Kwa kutumia mifano minne, jadili mtindo wa dondoo hili.** (alama 8)

- Methali (Kifo cha panzi furaha ya kunguru,)
- Swali balagha-(mnajua…?)
- Taswira -kijiduka uchwara hapa.
- Mazungumzo (Kesho mtamwona ameagiza vinywaji mbalimbali viletwe hapa muuziwe.)
- Usimulizi wa nafsi ya tatu (e. .amekuja hapa...)
- Usimulizi wa nafsi ya pili (mnajua... )

c) **Tathmini umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (alama 8)**

- Yanatusaidia kuelewa hasara za ubaguzi — Waketwa wanakosa makao.
- Yanamsaidia mwandishi kuj enga mtiririko wa vitushi kupitia Waketwa kuwa wakimbizi.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

- Yametusaidia kuelewa sifa za Mbwashu (mnafiki).
- Yanasaidia mwandishi kukuza mtindo kupitia mbinu ya mazungumzo.
- Tunaelewa suala la uongozi mbaya - Lesulia hawasaidii.
- Yanatujuza jinsi Mbwashu hunufaika kutokana na hasara yai Waketwa.
- Yanajenga suala la unafiki kupitia Nanzia ambaye anajifanya kuwa anawasaidia Waketwa kwa kuwaletea vyakula vya msaada.
- Yanachimuza ubadhirifu wa mali ya umma kupitia Mbwashu ambaye anabebwa kwa gari la serikali ilhali yeye si mfanyikazi wa serikali. (zozote 4x2)

**7.** 'Mwanamke ni musika mkuu katika kuibomoa jamii yake.'Jadili (alama 20)

1) Mbwashu anashirikiana na maafisa wa ngazi za juu serikalini kuagiza bidhaa ghushi bila kulipa ushuru.

2) Nanzia na Mbwashu wananyakua ardhi ya Matango.

3) Sihaba anakubali kuhongwa kwa kufanikisha kubatilishwa kwa ardhi ya Matango.

4) Sagilu ana uhusiano wa kimapenzi na Sihaba.

5) Nanzia anazini na Sagilu nje ya ndoa na kuzaa Ngoswe.

6) Mbungulu anakataza Mangwasha kuenda kumtafuta Mrima kwa sababu ya utamaduni potovu.

7) Sihaba anakuja na kifurushi chenye bomu kanisani.

8) Sihaba anashiriki katika kuchomwa kwa mtaa wa Matango.

9) Sihaba anasambaza vijikaratasi vya kuwaamrisha Waketwa wahame Matango

10) Sihaba anawatumia wasichana wadogo kama watumwa wa ngono.

12) Cheiya anajaribu kumuua Lonare kwa kumtilia sumu kwenye kinywaji.

13) Sagilu na Sihaba wanapanga kuhujumu biashara ya Lonare.

14) Akina mama wanaleta wasichana wao kwa Sihaba kufanya ukahaba ili walipwe.

15) Sihaba anatumika kutowesha washindani wa kibiashara wa Sagilu.

16) Nanzia ananyakua Skyline Mall kutoka kwa umma.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

17) Cheiya anazini na bamkwe mtarajiwa.

18) Cheiya anabadilika na kuanza kupenda pesa

19) Mbwashu anabebwa kwa gari la serikali ilhali yeye si mfanyikazi wa serikali; ubadhirifu..

20) Mangwasha anashuhudia wasichana wengi wakiwacha Shule na kuzamia mihadarati mitaani.

21) Mangwasha anashuhudia wasichana wadogo wakizaa watoto nje ya ndoa.

22) Mamapima anawauzia watu pombe haramu kule Ponda Mali. (zozote 10x2)

8.

a) Kichekesho -Ni mchezo mfupi ambao hupitisha ujumbe kwa njia au namna ya kuchekesha.(alama 2)

**b) Utanzu wa kipera hiki huweza kuchukua nafasi muhimu katika fasihi simulizi.**

**Thibitisha kwa hoja zozote sita AL 6**

-Huburudisha watazamaji na waigizaji wenyewe.

- Huhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii.

- Ni kitambulisho cha jamii.

- Hukuza umoja na ushirikiano wa watu wanapojumuika kushiriki katika vichekesho.

-Ni nyenzo za kupitisha maarifa na amali za jamii.

-Husawiri mtazamo wa jamii kuhusu masuala mbalimbali kama vile woga, wizi na usaliti.

- Hukuza ubunifu.

- Ni njia ya kuimarisha urafiki. Kwa vile mizaha na utani katika vichekesho hukuza urafiki na uhusiano bora

- Huongoza jamii kupambana na mazingira wanamojipata.

- Huelimisha kupitia maudhui na hulka za waigizaji .

**c) Ufanisi wa uwasilishaji wa utanzu huu unategenea fanani. Tetea kauli hii. (Alama 6)**

- Huwa mchangamfu na mcheshi kwa hadhira yake ili kuwafanya wapendezwe na hadithi
- Anafahamu utamaduni wa jamii yake.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

- Anaifahamu hadhira yake vizuri na kusimulia kulingana na mapendeleo yao. wasichana au wavulana? vijana au wazee?
- Huwa na uwezo wa ufaraguni - uwezo wa kubadilisha sehemu fulani za sanaa bila kujifunga na muundo asilia.
- Mwenye kumbukumbu nzuri - uwezo wa kukumbuka
- Mwenye uwezo wa kuigiza kwa kutumia viungo vyake, uso (ishara-uso) na sauti(kiimbo)
- Mwenye uwezo wa kujenga taharuki kwa kusita kidogo ili kuvuta nadhari ya hadhira yake.
- Hushirikisha hadhira yake katika nyimbo n.k
- Mtambaji hodari na mkwasi wa lugha.

**d) Ni changamoto zipi zinaweza kumkabili mwanafasihi nyanjani?( Alama 6)**

- Gharama ya utafiti-huenda gharama ikwa kubwa kiasi cha mtafiti kutoimudu. Baadhi ya mafanani au wahojiwa huenda wakadai walipwe kabla ya kutoa habari zozote.hivyo ikiwa mtafiti hana hela basi utafiti wake utakwamizwa.
- Mtazamo hasi wa wanajamii kuhusu ujazaji wa hojaji huenda ukawafanya wengi wao kutojaza hojaji zao. Wanajamii wengine huweza kushuku kwamba mtafiti anawapeleleza na wakakataa kutoa habari.
- Vizingiti vya kidini amabavyo hutokea pale ambapo baadhi ya wahojiwa wanaamini kwamba matendo ya fasihi simulizi.
- Uchache wa wazee au wataalamu wa fasihi simulizi ,kukosekana kwa wazee wanaoweza kutamba ngano ama kueleza vipera vingine k.v vitendawili.
- Matatizo ya mawasiliano na uchukuzi ikiwa mkusanyaji analazimika kwenda mbali kukusanya habari,hasa katika sehemu kame itakuwa vigumu iwapo hana gari.
- Ukosefu wa usalama ,huenda mkusanyaji wa fasihi simulizi akavamiwa ,baadhi ya watu si wakarimu na huenda wakamshuku mtafiti na kuvamiwa.
- Hali ya anga -mvua,jua kali n.k

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes